



SWAHILI A1 – STANDARD LEVEL – PAPER 2
SOUAHÉLI A1 – NIVEAU MOYEN – ÉPREUVE 2
SWAHILI A1 – NIVEL MEDIO – PRUEBA 2

Friday 18 May 2001 (morning)
Vendredi 18 mai 2001 (matin)
Viernes 18 de mayo de 2001 (mañana)

1 hour 30 minutes / 1 heure 30 minutes / 1 hora 30 minutos

INSTRUCTIONS TO CANDIDATES

- Do not open this examination paper until instructed to do so.
- Answer one essay question. You must base your answer on at least two of the Part 3 works you have studied. Substantial references to a Part 2 work of the same genre are permissible but only in addition to the minimum of two Part 3 works. References to other works are permissible but must not form the main body of your answer.

INSTRUCTIONS DESTINÉES AUX CANDIDATS

- Ne pas ouvrir cette épreuve avant d'y être autorisé.
- Traiter un sujet de composition. La composition doit être basée sur au moins deux des œuvres étudiées dans la troisième partie du cours. La composition peut comporter des références importantes à une œuvre du même genre étudiée dans la seconde partie, mais uniquement en plus des deux œuvres de la troisième partie. Les références à d'autres œuvres sont permises mais ne doivent pas constituer l'essentiel de la réponse.

INSTRUCCIONES PARA LOS ALUMNOS

- No abra esta prueba hasta que se lo autoricen.
- Elija un tema de redacción. Su respuesta debe basarse en al menos dos de las obras estudiadas para la Parte 3. Se podrán hacer referencias importantes a una obra de la Parte 2 del mismo género pero solamente como complemento a las dos obras de la Parte 3. Se permiten referencias a otras obras siempre que no formen la parte principal de la respuesta.

Andika insha juu ya moja ya masuala yafwatayo. Jibu lako liwe juu ya kazi mbili za Sehemu ya 3 ulizojifunza. Marejeo, kwa sehemu kubwa, ya kazi za Sehemu ya 2 za utanzu mmoja huohuo - yanaruhusiwa, lakini yawe tu kama ziada kwa uchache ya kazi mbili za Sehemu ya 3. Marejeo ya kazi nyengine yanaruhusiwa, lakini yasiwe msingi wa jibu lako.

Tamthilia

1. Ama

- (a) “Siasa inaweza kuwa au isiwe muhimu katika kazi ya fasihi. Jambo muhimu zaidi ni kwamba kazi ya fasihi lazima iwe imeandikwa kisanaa.” Onyesha vipi lugha imetumika kuwasilisha ujumbe wa waandishi hao kisanaa katika angalau kazi 2 ulizojifunza katika sehemu hii.

Au

- (b) Ukutumia angalau tamthilia 2 ulizojifunza katika sehemu hii, linganisha vipi waandishi wake wamefaulu kuwajenga wahusika wao wakuu.

Riwaya

2. Ama

- (a) Kwa kutumia mifano ya angalau kazi mbili ulizojifunza jadili vipi waandishi wake wanazingatia matatizo ya kijamii.

Au

- (b) “Usimulizi ni kipengele cha msingi katika riwaya yoyote ile, kiasi kwamba riwaya inayovutia ni ile ambayo mwandishi wake amefanikiwa mno katika usimulizi wake”. Jadili kauli hii kwa kuzingatia kazi 2 ulizojitayarisha nazo.

Ushairi

3. Ama

- (a) Zingatia miundo ya angalau tungo mbili za mashairi ya kazi ulizozisoma, kisha ujadili vipi mitindo ya miundo hiyo inavyosaidia kuimarisha uzuri na maana ya tungo hizo.

Au

- (b) Linganisha vipi dhamira za mashairi 2 ya kazi tofauti ulizozisoma zilivyowasilishwa kiufundi na washairi wake.

Riwaya ya Mapenzi

4. *Ama*

- (a) “Raha na mashaka ni sehemu ya mapenzi” - kutokana na angalau riwaya mbili ulizojitayarisha nazo, onyesha namna waandishi wake wanavyoonyesha uwili huu katika mapenzi.

Au

- (b) Kwa kutumia angalau mbili ya riwaya ulizojitayarisha nazo katika Sehemu ya 3, jadili namna gani matumizi ya lugha yanavyoimarisha ujumbe wanaotaka kuutoa kwa wasomaji wao.

Masuala ya Ujumla

5. *Ama*

- (a) Katika kazi angalau mbili ulizozisoma onyesha namna gani mwandishi anawapa kazi gani wahusika wake wakuu.

Au

- (b) “Jamii ni hazina kubwa ya mwandishi ambamo huchota mawazo yake.” Kwa kutumia angalau kazi mbili ulizojitayarisha nazo, jadili kwa kiasi gani mwandishi anajishughulisha na matatizo ya kijamii katika jamii yake.

Au

- (c) “Ingawa kazi za fasihi zinaakisi uhalisia wa maisha, si lazima uhalisi huo uwe mkavu au wenye mantiki tunayoilewa sisi.” Jadili, huku ukitoa mifano ya kazi mbili ulizozisoma.

Au

- (d) “Mwandishi anapaswa kuwa na uwezo mkubwa mno kuifinyaga lugha ili kuwavutia wasomaji wake.” Linganisha waandishi wawili wa kazi ulizojitayarisha nazo jinsi walivyofanikiwa kuitumia lugha ili kujenga mvuto.